



Watu wa aina tatu hatowasemesha Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama wala hatowatakasa na watakuwa na adhabu chungu

Na kutoka kwa Salmani Alfaaris -radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

"Watu wa aina tatu hatowasemesha Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama wala hatowatakasa na watakuwa na adhabu chungu, Mzee mzinifu, na masikini jeuri, na mtu aliyemfanya Mwenyezi Mungu kuwa ndio bidhaa, hauzi ila kwa kiapo chake wala hanunui ila kwa kiapo chake".

[Sahihi] [Imepokelewa Twabraniiy]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuhusu aina tatu za watu, wenye kustahiki adhabu ya Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama kwa adhabu tatu, endapo hawatotubia au kusamehewa adhabu: Ya kwanza: Hatowasemesha Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama kwa sababu ya ukali wa ghadhabu yake, bali atawapuza, au atawasemesha maneno yasiyowafurahisha na yanayoonyesha hasira yake juu yao. Ya pili: Hatowatakasa wala hatowasifia wala hatowasafisha kutokana na madhambi. Ya tatu: Watakuwa na adhabu yenye kuumiza sana Akhera. Na watu wa aina hiyo ni: Aina ya kwanza: Mtu mzima na anajiingiza katika machafu ya zinaa. Ya pili: Fakiri asiyekuwa na mali lakini pamoja na hivyo ana kiburi kwa watu. Ya tatu: Anayekithirisha kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu katika kuuza na kununua, analidhalilisha jina la Mwenyezi Mungu, na analifanya kuwa ndio nyenzo ya kujipatia mali.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/5952>

